**MAKUENI COUNTY CLUSTER PREPARATORY EXAMINATIONS 2016**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**JULAI/ AGOSTI 2016**

**MUDA: 2 ½**

**SEHEMU A: USHAIRI**

1. **LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia,namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

**Maswali**

(a) Shairi hili ni la kimapokea. Toa sababu mbili kuunga kauli hii. (Alama.2)
(b) Taja bahari kuu ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. Fafanua. (Alama.2)
(c) Fafanua dhamira ya mshairi. (Alama.2)
(d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (Alama.2)
(e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. (Alama.2)
(f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (Alama.4)
(g) Mshairi anamaanisha nini anaposema 'zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,' (Alama.2)
(h) Eleza toni ya shairi hili. (Alama.2)
(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao.
    i) Nitatongoa
    ii) Zitapusa. (Alama.2)

**SEHEMU YA B**
**TAMTHILIA**
**T. Arege; <u>Mstahiki Meya</u>**
***Jibu Swali la 2 au 3***

2. Huyo Meya wetu ana washauri ambao huwasikiliza zaidi hata kama wanampotosha. Fafanua. (Alama.20)

3. Mwafulani 1: Nilikusahau lini ndiyo sasa nije kukusahau?......"
   Mwafulani II: …..tusikie

(a) Eleza muktahda wa dondoo hili. (Alama.4)
(b) Bainisha mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. (Alama.2)
(c) Fafanua mambo yoyote **manne** yanayo zungumziwa na mwafulani wa pili kulingana na muktadha wa dondoo. (Alama.4)
(d) Fafanua maudhui yoyote **matano** yanayojitokeza kulingana na muktadha wa dondoo hili. (Alama.10)

for more past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

**SEHEMU C**
**Kidagaa Kimemwozea; Ken Walibora**
**Jibu Swali la 4 au 5**

4. Eleza jinsi mbinu ya kwelikinzani imetumika kwa kurejelea riwaya ya 'kidagaa kimemwozea. (Alama.20)

**5. Kidagaa Kimemwozea; Ken Walibora**
Ningemweka hai afikishwe mahakamani kweli idhihiri na uongo ujitenge".
(a) Eleza muktadha wa dondoo. (Alama.4)
(b) Fafanua kwa kutolea mifano ukweli wa kauli "kweli idhihiri". (Alama.6)
(c) Eleza hulka ya mnenaji. (Alama.4)
(d) Vitaje vitushi vyovyote **vitatu** vilivyomshangaza msemaji kulingana na muktadha wa dondoo. (Alama.6)

**SEHEMU YA D.**
**Hadithi fupi, Ken Walibora**
**6. Kanda la Usufi** - (R. Nyaga)
(a) Kanda la usufi ni anwani mwafaka.
Fafanua kwa kutolea mifano. (Alama.10)

(b) Lini angepata nafasi ya kupenya kwenye chungio…"
Fafanua jinsi msemewa angepata nafasi na changamoto zake. (Alama.10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**
**Jibu Swali la7 au 8.**
7. **i) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**
Mtu mmoja alimpa mke wake nambari yake ya simu. Kila mara bibi akipigia mumewe simu, ilipokelewa na sauti nyororo "mteja wa nambari uliopiga hapatikani kwa sasa." Alifunga safari kumtembelea mume wake mjini na kukabiliana na huyu kisura.

**MASWALI**
a) Bainisha kipera cha utungo huu. (Alama.2)
b) Onyesha sifa **tano** za kipera hiki. (Alama.5)
c) Eleza manufaa **tano** ya kipera hiki. (Alama.5)

**ii) Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali**
Ewe mpwa wangu,
Kwetu hakuna mwoga, usiwe kama msichana.
Uoga ukikufika, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume
Iwapo utatingiza kichwa
Uhamie kwa wasiokatwa
Waume wa mbari yetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo.

Simama jicho liwe juu
Ngariba alilala jikoni
Visu ametia makali
Kabiliana na kisu kikali
Wengi wasema ni kikali
Mbuzi utampata
Na hata shamba la mahindi
Usiende kwa wasiotahiri.

**MASWALI**
(a) Huu ni wimbo gani? Fafanua (Alama.2)
(b) Eleza shughuli **mbili** za kiuchumi zinazodokezwa na wimbo huu. (Alama.2)
(c) Onyesha taasubi ya kiume inavyojitokeza katika wimbo huu. (Alama.4)

8. a) Eleza mambo manne yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (Alama.8)
b) Eleza maana ya ngoma katika fasihi simulizi kisha utoe dhima zake nne. (Alama.5)
c) Eleza maana ya maapizo. (Alama.2)
d) matambiko ni nini? Eleza dhima zake mbili. (Alama.5)

for more past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479